**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

**HALMASHAURI YA WILAYA YA UYUI**

**Kumb.Na.HWU/A.30/63/52** **05/02/2026**

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Uyui anawatangazia Watanzania wenye sifa kuomba nafasi za kazi mbili (02) katika Halmashauri hii baada ya kupata kibali kutoka Ofisi ya Rais, Menejiment ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mchanganuo ufuatao:-

## 1.0. DEREVA WA MITAMBO II – NAFASI 2

### 1.1. MAJUKUMU NA KAZI

i. Kuendesha mitambo kikamilifu bila kusimamiwa.
ii. Kuweka vipimo mbalimbali vinavyotakiwa kufuatana na kazi anayofanya na jinsi anavyoelekezwa na kiongozi wa kazi hiyo.
iii. Kutoa huduma ya kwanza ya matengenezo ya mitambo na pia aweze kutoa maelekezo sahihi ya ubovu wa mitambo anapotakiwa kufanya hivyo.
iv. Kuandika vizuri 'log sheet' na kuweka kumbukumbu sahihi ya matumizi ya vifaa kwa mfano mafuta, grisi na vipuri.
v. Kuhakikisha kuwa mashine/mitambo inatumika kwa kazi zinazotakiwa.
vi. Kufanya usafi wa mtambo.
vii. Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na Msimamizi wake

#### 1.1.1. SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa mwenye elimu ya Kidato cha Nne (IV), leseni daraja 'G' ya uendeshaji mitambo pamoja na ujuzi wa kutunza vyombo mbalimbali vya mitambo hiyo awe na uzoefu wa kuendesha mitambo kwa muda usiopungua saa mia tatu (300) au miezi mitatu (3) bila kusababisha ajali

#### 1.1.2. NGAZI YA MSHAHARA

**TGOS A 1**

**MASHARTI YA JUMLA**

i. Waombaji wawe Watanzania wenye umri kuanzia Miaka **18** na usiozidi miaka **45**

ii. Waombaji waambatanishe maelezo binafsi yaliyojitosheleza Curriculum Vitae (CV) yenye Anuani inayotumika, namba ya simu zinazopatikana na Anuani ya barua pepe (E-mail address) pamoja na majina ya wadhamini (Referees) watatu wa kuaminika. "Provisional "Testimonials" Statement of results" na hati za matokeo za kidato cha Nne na Sita (Form IV na Form VI results slip **HAVITAKUBALIWA**

iii. Waombaji wote waambatanishe cheti cha kuzaliwa kilichothibitishwa na Mwanasheria/Wakili.

iv. Waombaji walio staafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana Kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.

v. Waombaji kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa Umma, wasiombe bali wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyo katika **Waraka Na.CAC.45/257/01/D/140 wa tarehe 30 Novemba, 2010.**

vi. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma vilivyo thibitishwa na Mwanasheria/Wakili ambavyo ni vyeti vya Kidato cha Nne,Kidato cha Sita kwa wale waliofikia kiwango cha vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika, kama vile.

vii. Postgraduate/Degree/Advanced Diploma/Diploma/Certificate, - Cheti cha mtihani wa Kidato cha IV Na Vi, - Computer Certificate – Vyeti vya kitaaluma (Professional Certificate from Respective Boards)

viii. Waombaji waliosoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vimethibitishwa na Mamlaka husika (**TCU, NECTA au NACTVET).**

ix. Uwasilishaji wa Taarifa na sifa za kughushi, wahusika watachukuliwa hatua za kisheria,

x. Barua ya maombi iandikwe kwa Kiswahili au Kingereza,

xi. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe **18 Februari ,2026,**

xii. **MUHIMU:** Kumbuka kuambatanisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu,aidha anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa:

**Mkurugenzi Mtendaji (W),**
**Halmashauri ya Wilaya ya Uyui,**
**S.L.P 610,**
**TABORA.**

xiii. Maombi yote ya kazi yatumwe kwenye mfumo wa kielektoniki wa ajira (Recruitment Portal) kupitia anuani ifuatavyo**;** [https://portal.ajira.go.tz](https://portal.ajira.go.tz) Anuani hii pia inapatikana

kwenye tovuti ya Sekretarieti ya Ajira kwa kuingia sehemu iliyoandikwa “Recruitment Portal”

xiv. Maombi yatakayo wasilishwa nje ya utaratibu ulioanishwa katika tangazo hili **HAYATAFIKIRIWA KABISA.**

**Limetolewa na:-**

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA UYUI**